SERA KWA KIFUPI

NI NAMNA GANI WANAWAKE NA VIJANA WENYE ULEMAVU WANAWEZA KUFIKIA HAKI ZA KIJINSIA NA AFYA YA UZAZI NA HAKI ZAO ZA KUISHI MAISHA YALIYO HURU DHIDI YA UKATILI KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA

©UNFPA Tanzania

1. Muhtasari

- Wanawake na vijana wenye ulemavu ni miongoni mwa watu wanaotengwa zaidi katika Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Ushahidi unaonesha kuwa haki zao za kijinsia na afya ya uzazi bado hazitekelezwi. Hali kadhalika, wanawake na vijana wenye ulemavu wanapitia kiwango kikubwa cha ukatili wa kijinsia..

- Nyenzo mbalimbali za kisheria na kisera, za kimataifa na kitaifa zinathibitisha kuwa watu wenye ulemavu wako sawa na wasio na ulemavu mbele ya sheria. Jumuiya ya kimataifa pia inazitaka nchi husika kuweka mifumo ya kisheria ya ulinzi kwa ajili ya watu wenye ulemavu ili kuhakikisha upatikanaji wa haki zao na kuwalinda; mitazamo hasi na unynyapaa kwenye jamii lazima vikabiliwe kwa kukuza uelewa, kuanzia katika ngazi ya familia.

- Mfumo kazi jumuishi wa kupinga ukatili wa kijinsia na kuhakikisha upatikanaji wa haki za kijinsia na afya ya uzazi; unaozingatia haki, usawa wa kijinsia na unaochochea mabadiliko ya kijamii ni muhimu.

2. Utangulizi

Kusudi la ufupisho huu wa sera ni kutoa taarifa zitakazotumika kwenye utetezi, utafutaji wa rasilimali, na kuwezesha huduma zinazofikika ili kuhakikisha wanawake na vijana wenye ulemavu wanaweza kufikia haki zao za kijinsia na afya ya uzazi na haki ya kuishi maisha yaliyo huru dhidi ya ukatili.

Watu wenye ulemavu hujumuisha walio na changamoto za kimwili, kiakili, na kihisia za muda mrefu ambazo zinapoingiliana na vikwazo vya kimitazamo, kimazingira na na kitaasisi hufanya iwe vigumu kwao kushiriki kikamilifu na kwa ufanisi katika shughuli za jamii sawasawa na wengine. Shirika la afya duniani linakadiria kuwa duniani kote zaidi ya watu bilioni moja wanaishi na aina fulani ya ulemavu – karibu sehemu moja ya tano wakiwa wanawake Hii inakadiriwa kuwa 15% ya ya wakazi wa dunia, wakiwemo 190 milioni (3.8%) walio na umri wa miak 15 na zaidi wenye changamoto kubwa katika kushiriki shughuli za kila siku.

SERA KWA KIFUPI.pdf 2 11/28/2021 11:04:31 PM

Katika Tanzania bara, **takwimu za watu wenye ulemavu** ni 6.8% (5.7% kwa wanaume na 7.8% kwa wanawake), wakati visiwani Zanzibar takwimu ni 3.2% (3.3% kwa wanaume na 4.1% kwa wanawake). Takwimu hizi ni chini ya wastani wa kidunia kwa mujibu wa Shirika la Afya duniani na zinaweza kuwa matokeo ya watu wengi wenye ulemavu kutokutolewa taarifa kwa sababu ya unyanyapaa dhidi ya ulemavu. Takwimu za ulemavu ziko juu zaidi maeneo ya vijijini ukilinganisha na mijini.

Nchini Tanzania, watu wenye ulemavu ni miongoni mwa maskini zaidi na waliotengwa kwenye jamii. Haijalishi mahali wanapoishi au jinsi zao, watu wenye ulemavu wana uwezekano mkubwa zaidi wa kukosa ajira, kutokujua kusoma, kuwa na viwango vya chini vya elimu rasmi, na uwezekano mdogo zaidi wa kupata mtandao wa msaada na mtaji wa kijamii ukilinganisha na watu wasio na ulemavu.

Haki za kijinsia na afya ya uzazi zinahusiana na hali ya utimamu, kimwili, kihisia, kiakili na kijamii katika nyanja zote za kijinsia na uzazi, na wala sio tu kutokuwepo kwa magonjwa au changamoto (Mpango wa Utekelezaji wa Mkutano Wa Kimataifa wa Idadi ya Watu na Maendeleo (1994)) . Watu wenye ulemavu wana mahitaji ya kijinsia na afya ya uzazi ya kipekee na mara nyingine ya ziada. Kutengwa kwao huzidi kuongezeka pale wanapokumbana na vikwazo katika upatikanaji wa taarifa, elimu na huduma za kijinsia na afya ya uzazi ambazo zinajitosheleza, zenye kina na zinazotolewa kwa namna ya heshima. Hali hii hupelekea kuwa na idadi ya kubwa ya mimba zitokanazo na ukatili wa kingono, maambukizi ya VVU au magonjwa ya zinaa vyote vikiingiliana na mazingira ya unyanyapaa. Watu wenye ulemavu wana uwezekano mkubwa wa kupitia changamoto katika upatikanaji wa huduma za kijinsia na afya uzazi, kwa sababu ya kutokufikika kwa miundombinu, vikwazo vya mawasiliano, mitazamo hasi ya watoa huduma, kukosekana kwa usiri, gharama za huduma, kutendewa vibaya na kutokujitosheleza kwa huduma zitolewazo.

Tafiti nyingi zinaonyesha uwepo wa viwango vya juu vya ukatili wa kijinsia dhidi ya watu wenye ulemavu. Ukatili wa kijinsia ni vitendo ya ukatili (wa kimwili, kihisia, kisaikolojia, kingono na kiuchumi) yatendwayo bila ridhaa ya mtu kwa kigezo cha tofauti za kijinsia baina ya wanawake na wanaume. Wasichana na wanawake wenye ulemavu wana uwezekano mkubwa zaidi wa kupitia vitendo vya ukatili wa kingono na dhuluma dhidi yao kwa sababu ya ulemavu wao. Janga la UVIKO-19 limeongeza hatari ya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na wasichana wenye ulemavu. Mara nyingi matukio ya ukatili wa kijinsia dhidi ya watu wenye ulemavu hayatolewi taarifa kwa mamlaka husika kwa sababu ya utegemezi kwa walezi wao, kawaida za kijamii zinazohusudisha walezi wa watu wenye ulemavu na hivyo kuwalinda

SERA KWA KIFUPI.pdf 3 11/28/2021 11:04:31 PM

wafanya makosa ndani ya familia; ukosefu wa usiri na utunzaji wa taarifa binafsi; wafanyamakosa kutoshtakiwa na hivyo kukosekana kwa imani kwenye huduma za kitaaluma na mifumo ya kisheria, huduma za kisheria kutokuwa rafiki kwa watu wenye ulemavu na unyanyapaa dhidi ya jinsia na watu wenye ulemavu.

Kawaida za kijinsia na kijamii zina athari kubwa katika maisha ya wanawake na vijana wenye ulemavu. Ulemavu, jinsi na umri vinahusiana na kawaida mbalimbali za kijamii na hivyo muingiliano wa vyote viwili huunda namna za kipekee za ubaguzi na kuongeza hatari ya ukatili. Kawaida za kijamii zinachochea kukubalika kwa ubaguzi na ukatili dhidi wanawake wenye ulemavu. Kawaida za kitamaduni na kijamii mara nyingi huwaona watu wenye ulemavu kama wasio na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya miili na afya zao. Licha ya ushahidi kuonyesha kuwa vijana wenye ulemavu hushiriki ngono sawasawa na wenzao wasio na ulemavu, wao huchukuliwa kama watu wasio na hitaji la taarifa sahihi za afya ya uzazi. Hali hii huongezewa uzito na imani kuwa watu wenye ulemavu hawashiriki vitendo vya ngono na hawawezi kupata watoto, na hivyo mara nyingi huwekwa kando kwenye huduma za afya ya uzazi.

3. Mfumo kazi wa Kimataifa wa Haki za Kibinadamu

Nyenzo mbali mbali za kimataifa zinaunda mfumokazi wa kiulimwengu wa haki za binadamu na kuainisha wajibu wa **kuheshimu, kulinda na kutimiza** haki za afya ya uzazi za watu wenye ulemavu. Makubaliano muhimu ya kimataifa yanayohusiana na **haki za afya ya uzazi na ulinzi dhidi ya ukatili wa kijinsia** kwa wanawake na vijana wenye ulemavu yameorodheshwa hapa chini.

- **Mkataba wa Haki za Watu Wenye Ulemavu: Jamhuri** *Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilisaini mkataba huu mwezi wa tatu mwaka 2007 na kuuthibithisha mwaka 2009.*
- **Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake:** *Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilisaini mkataba huu mwaka 1985 na kuuthibithisha mwaka 1986.*
- **Mkataba wa Haki za Mtoto:** *Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilisaini mkataba huu mwezi wa sita mwaka 1990 na kuuthibithisha mwaka 1991.*
- **Mpango wa Utekelezaji wa Mkutano wa Kimataifa wa Idadi ya Watu na Makazi (1994) na Tamko la Maazimio 25 ya ICPD, Nairobi mwaka 2019: Kuongeza kasi ya Kuifikia Ahadi.**
- **Malengo ya Maendeleo Endelevu.**

SERA KWA KIFUPI.pdf 4
11/28/2021 11:04:32 PM

4. Mifumo kazi ya Kisheria na Kisera katika Ngazi ya Taifa

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 zinaainisha haki za msingi za watu wote lakini hazitaji kwa upekee wake haki za msingi za watu wenye ulemavu. Katika mtazamo wa kisera, serikali ya Tanzania iliunda Mkakati wa Kitaifa wa Ujumuishi wa mwaka 2010 hadi 2015 na Sera ya Taifa ya Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2004 kwa Tanzania bara na Sera ya Kitaifa ya Ulemavu ya mwaka 2018 kwa upande wa Zanzibar.

Kuhusiana na hatua za kisheria sehemu zote mbili za Muungano (Tanzania bara na visiwani) vimeunda sheria maalum za ulemavu. **Sheria ya Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2010** kwa Tanzania bara na **Sheria ya Watu wenye Ulemavu (Haki na Fursa) ya mwaka 2006 kwa Zanzibar.**

Mbali na kuainisha haki na wajibu kuhusiana na ulemavu, sheria hizi zinaweka taratibu za utekelezaji ikiwa ni pamoja na mabaraza ya ushauri kama inavyotakiwa na ibara namba 33 ya Mkataba wa Haki za Watu wenye Ulemavu. Kifungu cha saba ya sheria ya watu wenye ulemavu kwa Tanzania bara kimesimamia uanzishaji wa **Baraza la Kitaifa la Ushauri** la watu wenye ulemavu; sheria ihusianayo na ulemavu ya Zanzibar pia inatoa maelekezo ya uanzishwaji wa baraza kama hilo. Serikali zote mbili zimeunda **idara maalum ya ulemavu** katika ofisi ya Waziri Mkuu kwa Tanzania bara; na Baraza la Kitaifa la Ulemavu katika ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais wa Zanzibar.

Kwenye masuala ya ufikikaji wa huduma za afya, likiwemo suala la haki za kijinsia na afya ya uzazi na ukatili wa kijinsia, Tanzania bara iliunda **Mpango wa Kitaifa wa Hatua Dhidi ya Ukatili kwa Wanawake na Watoto (2017/18-2021/22)** ambao kusudi lake ni kuimarisha mwitikio wa mfumo wa kisheria kwa mahitaji ya makundi yaliyoko hatarini kama wanawake na wasichana wenye ulemavu. Tanzania bara pia iliunda **Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya** ambao unatoa mwongozo wa ufikikaji wa huduma za msingi za afya. Visiwani Zanzibar, **Mpango wa Kitaifa wa Hatua Dhidi ya Ukatili kwa Wanawake na Watoto (2017-2022)** umejikita katika upatikanaji wa elimu ya msingi na jitihada za kuchukuliwa kwa hatua za mapema katika kuzuia ukatili na kuitikia vitendo vya ukatili. **Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya sehemu ya tatu wa Zanzibar (2013/14- 2018/19)** umejumuisha baadhi ya hatua madhubuti zitakazochukuliwa mf. kukabiliana na utapiamlo ambazo zinaweza kuwanufaisha watoto na wanawake wenye ulemavu.

SERA KWA KIFUPI.pdf 5 11/28/2021 11:04:32 PM

5. Mfumo kazi wa hatua za baadaye

Jedwali lifuatalo hapa chini linatoa mfumo kazi wa hatua za kuchukua ili kufanikisha utoaji huduma za haki za afya ya uzazi na kuzuia na kuitkia vitendo vya ukatili wa kijinsia zinazozingatia haki na zenye kubadilisha mazoea ya kijamii kuhusu wanawake na vijana wenye ulemavu.

MIONGOZO YA MSINGI YA HATUA ZA KUCHUKULIWA		
1. Kutengeneza mazingira ya sera na sheria wezeshi a. Tathmini na ufuatiliaji wa mazingira ya kisheria b. Ushawishi na utetezi wa kisheria c. Sera na mipango ya kitaifa	2. Uundaji, Utekelezaji na Ufuatiliaji wa Programu a. Ushirikishwaji wa wanawake na vijana wenye ulemavu b. Ushirikishwaji wa viongozi na taasisi za kidini, viongozi wa kijamii na wa kimila c. Kujenga uwezo d. Utekelezaji wa Programu e. Huduma zilizopo f. Ufanisi katika utambuzi wa mahitaji na huduma za rufaa g. Huduma zinazofikika h. Huduma zinazokubalika i. Huduma bora j. Huduma zinazozingatia misingi ya haki k. Ukusanyaji wa taarifa na ufuatiliaji	3. Vituo vya huduma vinavyofikika a. Kutambua vikwazo b. Ufikikaji wa miundo mbinu c. Ufikikaji wa kihisia d. Ufikikaji wa taarifa na miundombinu e. Ufikikaji kiuchumi

Huduma za Ukatili wa Kijinsia	Huduma za Ujinsia na Afya ya Uzazi
1. Kuzuia ukatili wa kijnsia 2. Huduma za afya kwa wahanga na wanusurika wa ukatili wa kijinsia 3. Huduma za haki na kipolisi 4. Huduma za kijamii – Huduma za ulinzi 5. Huduma za kijamii – Huduma za utengamao 6. Huduma za ukatili wa kijinsia kwa wanawake na vijana wenye ulemavu walio kwenye mazingira ya taasisi 7. Huduma za Ukatili wa kijinsia ambazo ni rafiki kwa vijana na rika la balehe	1. Taarifa, bidhaa na huduma za kupanga uzazi 2. Huduma za kujifungua na mtoto mchanga 3. Elimu na taarifa za ujinsia za kina na kujitosheleza 4. Taarifa, upimaji na huduma za matibabu ya magonjwa ya zinaa pamoja na VVU 5. Kupata taarifa na huduma za afya kwa namna sawa na wengine 6. Taarifa na huduma ambazo ni rafiki kwa vijana na rika la balehe

SERA KWA KIFUPI.pdf 6

11/28/2021 11:04:33 PM

6. Hatua za msingi

Kuhakikisha wanawake na vijana wenye ulemavu wanapata haki zao za afya ya uzazi

- Kuwashirikisha wanawake na vijana wenye ulemavu kwenye utunzi wa sheria, sera na mipango kazi ya huduma za afya na huduma za afya ya uzazi.
- Kufanya tathmini ya wigo wote wa ufikikaji wa huduma katika vituo vya huduma ya kijinsia na afya ya uzazi.
- Kuandaa mpango kazi wa kushughulikia mapungufu kwenye ufikikaji wa huduma.
- Kutoa mwongozo kwa watoa huduma wa afya ya uzazi juu ya namna wanavyoweza kuhakikisha kuwa vituo vya huduma na vifaatiba vinafikika kwa watu wenye ulemavu, huduma na bidhaa zinafikika kiuchumi, wagonjwa wanapewa taarifa kwa namna inayofikika na watafsiri wa lugha ya alama na wasaidizi wengine waliopata mafunzo wanapatikana.
- Kuhakikisha kuwa watoa huduma wa kijinsia na afya ya uzazi na wafanyakazi wao wanapata mafunzo juu ya haki za binadamu, hususani haki za kijinsia na watu wenye ulemavu ikiwa ni sehemu ya mafunzo yao ya kitabibu. Hii inajumuisha kuelewa jukumu la wasaidizi wakati wa kupokea huduma, pamoja na wakati ambapo tahadhari za kujikinga dhidi ya UVIKO 19 zimewekwa.
- Kuhakikisha kuwa wafanyakazi katika vituo vya huduma ya afya ya uzazi wamepata mafunzo ya huduma bora na zinazozingatia haki za binadamu kwa watu wenye ulemavu na namna ya kuwasiliana na kufanya kazi na watu wenye ulemavu moja kwa moja ili kufuatilia viashiria vya ukatili.

Kuzuia na kushughulikia ukatili wa kijinsia kwa wanawake na vijana wenye ulemavu

- Kuwashirikisha ipasavyo wanawake na vijana wenye ulemavu katika utengenezaji, utekelezaji na ufuatiliaji wa mipango na sera za kitaifa zihusianazo na ukatili wa kijinsia. Kuhusianisha sera na mipango hiyo na uwezeshaji kiuchumi.
- Kujenga mwitikio wa pamoja wa sekta mbalimbali dhidi ya ukatili wa kijinsia unaoongeza kiwango cha usalama na usaidizi kwa wahanga na wanusurika wa ukatili wa kijinsia kupitia mfumo kazi imara, wa haraka na endelevu unaoleta matokeo ya kudumu na endelevu na kujenga utamaduni wa kitaasisi na kijamii kuwa ukatili wa kijinsia dhidi ya watu wenye ulemavu haukubaliki na hauvumiliki.
- Kutambua kwenye sheria, sera na mipango kazi kuwa wanawake na vijana wenye ulemavu wanaweza kupitia aina za ukatili wa kijinsia zinazofanana na wengine na pia kupitia aina za pekee za ukatili, kama vile ukatili unaofanywa na walezi au wasaidizi, au kunyimwa kwa dawa, vifaa saidizi au usaidizi kwenye shughuli za kila siku, na hizi aina zote za ukatili ziainishwe kwenye tafsiri ya ukatili wa kijinsia.

SERA KWA KIFUPI.pdf 7 11/28/2021 11:04:33 PM

- Kuweka rejea za wazi kwenye Mipango ya Kitaifa ya Hatua za Kukomesha Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto ambazo zinahusiana moja kwa moja na kushughulika na ukatili wa kijisia wanaofanyiwa wanawake na vijana wenye ulemavu. Hii ni pamoja kuweka mpango wa kuhakikisha upatikanaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu katika kipindi cha marufuku za kutotoka nje au dharura zingine zinazozuia watu kutoka sehemu moja kwenda nyingine (kama janga la UVIKO 19). Mipango ya Kitaifa ya Hatua za Kukomesha Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto ijumuishe ufuatiliaji wa taasisi za makazi na kuanzisha mifumo ya utoaji taarifa inayokubalika na kufikika ili kuhakikisha wakazi wote taasisi hizi wanapata haki zao za kuwa salama na kutunziwa siri zao.
- Kuunda mifumo ya uwajibikaji na ufadhili ili kuhakikisha ufanisi wa sheria, sera na mipango kazi ikiwemo ufuatiliaji wa utoaji huduma za usaidizi kwa wahanga wa ukatili wa kijinsia.
- Kuhakikisha kuwa kuna sera na utaratibu salama na usio wa ubaguzi wa upimaji wa awali wa watu wenye ulemavu wanaopokea huduma za afya ya uzazi ili kutambua ikiwa wanapitia ukatili wa kijinsia, ikiwemo kuwapa rufaa kwenda kwenye huduma zinazokubalika na kufikika na utoaji wa matibabu unaozingatia mtazamo wa kumsikiliza na kumjali mnusurika.

Kuimarisha upatikanaji wa takwimu na tafiti ili kuwezesha mjadala wa sera na kuunda programu

- Kukusanya taarifa za kitakwimu zinazoweza kutenganishwa kwa aina za ukatili wa kijinsia na ulemavu. Hii itawezesha uelewa bora zaidi wa namna uzoefu wa wanawake na vijana wenye ulemavu unavyoingiliana na aina mbalimbali za ukatili wa kijinsia. Hii inaweza kuwa pamoja na kujumuisha maswali ya "Washington Group" juu ya ulemavu katika tafiti za masuala ya Kidemografia na Afya na tafiti za ukatili dhidi ya watoto zinazofanywa nchini Tanzania. Takwimu za tafiti mbalimbali zinazoweza kulinganishwa ni muhimu ili kuwezesha uandaaji wa programu na sera zinazofikia mahitaji kwa ukamilifu.
- Kutenganisha takwimu za huduma za afya ili kuweza kuelewa upatikanaji wa huduma husika. Tafiti zinaweza kusaidia kuelezea namna vikwazo katika ufikikaji wa huduma vinaweza kuwa na athari katika ujinsia na afya ya uzazi na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na vijana wenye ulemavu ili kutoa taarifa zitakazowezesha uandaji wa programu na sera zitakazozingatia muktadha husika na kuondoa vikwazo.
- Ushiriki wa watu wenye ulemavu katika tafiti zinazowahusu ni muhimu ili kuhakikisha wananufaika kikamilifu kutoka kwenye tafiti husika

SERA KWA KIFUPI.pdf 8
11/28/2021 11:04:34 PM

Kupatanisha kawaida za kijamii na haki za afya ya uzazi na utu wa wanawake na vijana wenye ulemavu

- Kusisitiza namna ambavyo mifumo thabititi ya haki za afya ya uzazi, ikiwemo ufikikaji wa huduma za afya za uzazi na huduma za kuzuia na kuitikia vitendo vya ukatili wa kijinsia inavyoweza kunufaisha jamii nzima hususani wanawake na wasichana.
- Kuangazia namna uwezo wa kutekeleza haki za uzazi, ufikikaji wa huduma za afya ya uzazi na huduma jumuishi za kuzuia na kuitikia vitendo vya ukatili wa kijinsia vitaboresha afya, elimu na shughuli za kiuchumi kwa wanawake na vijana wenye ulemavu.
- Kuelimisha viongozi wa kijamii na wa kidini kuhusu ulemavu na faida za upatikanaji wa taarifa na huduma za haki za afya ya uzazi kwa familia na jamii. Kuendesha kampeni za kuongeza uelewa wa jamii kuhusu athari za ukatili wa kijinsia kwa watu wenye ulemavu ikiwemo katika maeneo ya vijijini.
- Kujumuisha katika kampeni hizi taarifa juu ya ukatili wa kijinsia unaofanywa dhidi ya wanawake na vijana wenye ulemavu na haki zao, na taarifa juu ya huduma za usaidizi wa ukatili wa kijinsia na watu walioko hatarini wanavyoweza kutafuta msaada. Kampeni zinapaswa kutoa taarifa zinazoendana na umri husika na zinazowaonesha wanawake na vijana wenye ulemavu katika mtazamo chanya.
- Kutoa taarifa kuhusu ukatili wa kijinisa katika mifumo kadhaa inayofikika kwa watu wenye ulemavu (taarifa za kidijitali zinazofikika, maandishi ya wasioona, lugha ya alama, na maandiko ya lugha rahisi)
- Kuimarisha uwezo wa vyombo vya habari kufanya jumbe zao kuwa zinazofikika na zinazoeleweka, ili watu wenye ulemavu wawe na ufahamu juu ya haki zao za ujinsia na afya ya uzazi.
- Kuhamasisha vyombo vya habari juu ya wajibu wao katika kusaidia kutekelezwa kwa haki za afya ya uzazi za watu wenye ulemavu na haki yao ya kuishi maisha yaliyop huru dhidi ya ukatili wa kijinsia , ikiwa ni pamoja na kuweza kufikia huduma za kuzuia na kuitikia vitendo vya ukatili wa kijinsia.
- Kukuza uelewa wa wanataaluma wa habari juu ya lugha wasiliani jumuishi kwa watu wenye ulemavu na yenye heshima, isiyoendeleza mitazamo hasi kuhusu watu wenye ulemavu.

Kutafuta rasilimali za ndani na nje ya nchi na kuongeza usaidizi wa kitaalam

- Kuonesha umuhimu wa kuhakikisha huduma za afya ya uzazi na programu za kuzuia na kuitikia vitendo vya ukatili wa kijinsia zinafikika kabisa, ni jumuishi, zinazozuia ubaguzi, ukatili na matokeo hafifu ya ujinsia na afya ya uzazi kwa wanawake na vijana wenye ulemavu.
- Kuangazia mapungufu katika ujuzi, uwezo usiojitosheleza wa watoa huduma na ukosefu wa rasilimali muhimu, ambavyo vinafifiisha uwezo wa watu wenye ulemavu kufikia haki zao za afya ya uzazi kikamilifu na kulindwa dhidi ya ukatili wa kijinsia.

SERA KWA KIFUPI.pdf 9 11/28/2021 11:04:35 PM

- Kuonesha namna upanuzi wa ufikikaji wa huduma za afya ya uzazi na huduma za kuzuia na kuitikia vitendo vya ukatili wa kijinsia vinavyoweza kuwa na jukumu chanya katika kulinda haki za afya ya uzazi, kuboresha afya, elimu na ushiriki katika shughuli za kuingiza kipato kwa wanawake na vijana wenye ulemavu.
- Kuonesha hitaji la kuongeza ufadhili kwa ajili ya miradi inayohusiana na haki za afya ya uzazi na huduma za kuzuia na kuitikia ukatili wa kijinsia ikiwa ni pamoja na kutanua wigo wa ufikikaji wa huduma.

7. Rejea

- Bowen, Erica, and Charlotte Swift. "The Prevalence and Correlates of Partner Violence Used and Experienced by Adults with Intellectual Disabilities: A Systematic Review and Call to Action". ["Takwimu na Visababishi vya Ukatili wa Wenzi kwa Watu Wazima wenye Ulemavu wa Kiakili: Mapitio ya Maandiko na wito wa Kuchukua Hatua."] Trauma, Violence, & Abuse 20, No. 5 (2019): 693–705. doi:10.1177/1524838017728707.
- Casebolt, M. Tara. "Barriers to Reproductive Health Services for Women with Disability in Low- and Middle-income Countries: A Review of the Literature". ["Vikwazo vya upatikanaji wa Huduma za Afya ya Uzazi katika Nchi za Kipato cha Chini na cha Kati: Mapitio ya Maandiko"] Sexual & Reproductive Healthcare 24 (2020): 100485. doi:10.1016/j.srhc.2020.100485.
- Chirwa, Esnat, Rachel Jewkes, Ingrid Van Der Heijden, and Kristin Dunkle. "Intimate Partner Violence Among Women With and Without Disabilities: A Pooled Analysis of Baseline Data from Seven Violence Prevention Programmes". ["Ukatili wa Wenzi Miongoni mwa Wanawake wenye Ulemavu na Wasio na Ulemavu: Mchanganuo wa Takwimu kiutoka katika Programu Saba za Kuzuia Ukatili"] BMJ Global Health 5, No. 11 (2020): e002156. doi:10.1136/bmjgh-2019-002156.
- Government of the United Republic of Tanzania, National Plan of Action to End Violence Against Women and Children [Mpango wa Kitaifa wa Kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto] 2017/18 – 2021/22.
- Hameed S, Maddams A, Lowe H, et al. From words to actions: Systematic review of interventions to promote sexual and reproductive health of persons with disabilities in low- and middle-income countries. [Kutoka Maneno hadi Vitendo: Tathmini ya Hatua za Kuboresha ujinsia na Afya ya Uzazi kwa Watu wenye Ulemavu katika Nchi za Kipato cha Chini na cha Kati] BMJ Global Health 2020;5:e002903. doi:10.1136/ bmjgh-2020-002903.
- Mesiäislehto V, Katsui H, Sambaiga R. Disparities in Accessing Sexual and Reproductive Health Services at the Intersection of Disability and Female Adolescence in Tanzania.[Mapungufu katika Upatikanaji wa Huduma za Ujinsia na Afya ya Uzazi pale Ulemavu na Balehe kwa Wasichana Vinapoingiliana Nchini Tanzania] Int J Environ Res Public Health. (2021); 18(4):1657. doi: 10.3390/ ijerph18041657. PMID: 33572337; PMCID: PMC7916121.
- Revolutionary Government of Zanzibar, National Plan of Action to End Violence Against Women and Children [Mpango wa Kitaifa wa Kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto] 2017/18 – 2021/22
- UN General Assembly, Note by the Secretary-General (2017) Sexual and reproductive health and rights of girls and young women with disabilities [Hotuba ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (2017) Haki za Ujinsia na Afya ya Uzazi kwa Wasichana na Wanawake wa Makamo wenye Ulemavu) Note by the Secretary-General https://undocs.org/en/A/72/133
- UNFPA. "Women and Young People with Disabilities: Guidelines for Providing Rights-Based and Gender-Responsive Services to Address Gender-Based Violence and Sexual and Reproductive Health and Rights". ["Wanawake na Vijana wenye Ulemavu: Muongozo wa Utoaji Huduma Zinazoshughulikia Ukatili wa Kijinsia na Haki za Ujinsia na Afya ya Uzazi Zinazozingatia Haki na Mahitaji ya Kijinsia"] United Nations Population Fund: New York (2018).
- UNFPA. "Young Persons with Disabilities. Global Study on Ending Gender-Based Violence and Realizing Sexual and Reproductive Health and Rights". ["Vijana wenye Ulemavu. Utafiti wa Kiulimwengu wa namna ya Kukomesha Ukatili wa Kijinsia na Utekelezaji wa Haki za Ujinsia na Afya ya Uzazi"] United Nations Population Fund: New York (2018).

SERA KWA KIFUPI.pdf 10

11/28/2021 11:04:35 PM